HakiElimu
Education Brief Na.07.2K

# Ruzuku Maalumu kwa Wanafunzi wa Elimu ya Msingi

## Changamoto na Mapendekezo kwa Ajili ya Uboreshaji

**Usuli**
Ruzuku maalumu kwa kila mwanafunzi wa elimu ya msingi imekusudiwa kutoa fedha kwa ajili ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wanaoandikishwa katika Shule za Serikali. Mfuko huu umeleta tofauti kubwa katika ngazi ya shule.

Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM) umeweka kiwango cha ruzuku maalumu kwa kila Mwanafunzi kuwa Dola 10 za Kimarekani (karibu kiasi cha shilingi za Kitanzania 12,500 kwa kutumia kiwango cha ubadilishaji fedha cha sasa) kwa mwanafunzi.[i]

**Mfuko wa Ruzuku Maalumu kwa kila Mwanafunzi hufanya nini?**

- Matengenezo ya vifaa
- Vitabu vya kiada, miongozo ya kufundishia,vifaa vya ziada vya kusomea
- Chaki, madaftari, kalamu, penseli
- Vifaa vya utawala
- Karatasi za mitihani, manunuzi na uchapaji

Fedha za Ruzuku Maalumu kwa kila Mwanafunzi huhamishwa kutoka Serikali Kuu kwenda kwenye kila mamlaka ya Serikali za Mitaa (LGA), ambazo huzipeleka fedha hizo kwenye akaunti za shule.[ii] Wizara tatu tofauti – Wizara ya Fedha, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (MOEVT), na Ofisi ya Waziri Mkuu – Tawala za Mikoa na Serikali za Mtaa (TAMISEMI) – zinahusishwa, kwa vile kiasi fulani cha ruzuku maalumu kwa kila mwanafunzi hugharimiwa na Mfuko wa Jumla wa Elimu. Na kiasi kingine hugharimiwa na huhamishwa kutoka MOEVT. Mikoa pia inahusika, ikifanya mfumo wa ulipaji uwe wenye utata wa hali ya juu.[iii]

**Changamoto**
Tangu kuanzishwa kwa MMEM, ruzuku maalumu kwa kila mwanafunzi zimeongeza ubora wa mafunzo kwa kuzipatia shule rasilimali zinazohitajika. Hata hivyo, bado kuna changamoto dhahiri.

***1. Ruzuku maalumu kwa kila mwanafunzi imekuwa inatolewa pungufu.***
Kiwango kamili cha fedha za ruzuku maalumu kwa kila mwanafunzi hakikuwa kikizifikia shule kwa wakati unaotakiwa. Uchunguzi wa kufuatilia matumizi ya umma wa 2004 (PETS) uliosimamiwa na

REPOA uligundua kwamba 40% ya rasilimali za ruzuku maalumu kwa kila mwanafunzi haikufika ngazi ya shule kwa wakati muafaka. Taarifa ya Maendeleo ya Serikali ya hivi karibuni inaeleza kwamba kati ya Julai 2005 na Juni 2006, 92% ya kima lengwa kilipelekwa mashuleni.

***2. Ulipaji umekuwa hautabiriki na unaotofautiana.***
PETS ya 2004 ilibaini tofauti kubwa miongoni mwa shule sampuli, baadhi ya shule zikipata kiasi karibu mara tatu zaidi kuliko wanafunzi wa shule nyingine. Zaidi ya hayo, fomula tofauti zinatumika kukokotoa vipengele tofauti vya ruzuku maalumu kwa kila mwanafunzi. Mgao wa Mfuko wa Pamoja wa Elimu kwa kila wilaya hukokotolewa kwa msingi wa watoto waliofikia umri wa kwenda shule katika wilaya. lakini wilaya huagizwa na Wizara ya TAMISEMI kusambaza rasilimali za kiwango cha shule kwa kuzingatia idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika kila shule (kwa mujibu wa makadirio ya sera ya MMEM ya Wizara ya Elimu).[iv]

***3. Mfumo tata wa malipo.***
Uhusishaji wa wizara tatu tofauti na ukosefu wa utaratibu wazi wa utoaji wa taarifa hufanya iwe vigumu sana kufuatilia fedha za ruzuku maalumu kwa kila kila mwanafunzi na kuamua iwapo ruzuku hiyo inazifikia shule hasa.

Mfano wa hivi karibuni unaonesha changamoto hizi zinazoingiliana. Mwezi Februari, 2007 Wizara ya Elimu ilichapisha taarifa katika magazeti ya kitaifa kuhusu kiasi cha ruzuku maalumu kwa kila mwanafunzi cha MMEM kilichopelekwa kila wilaya kwa ajili ya mwaka '2006/7'. Tangazo hilo la gazeti halikueleza iwapo hayo yalikuwa malipo ya mwanzo, ya pili, ya tatu au malipo pekee kwa mwaka huo wa fedha; iwapo malipo mengine yangefuatia au kutoa taarifa zozote zaidi. Data hiyo iliyochapishwa ilionesha tofauti kubwa baina ya kiasi kwa kila

mwanafunzi, ambazo hazikufuata mpangilio wowote unaofahamika.

Wastani wa kiwango kilichopelekwa kupitia ulipaji huu ulikuwa shs. 2,705 tu kwa mwanafunzi au kiasi cha 21% ya ruzuku maalumu yote kwa kila mwanafunzi. Zaidi ya hayo, hilo tangazo la gazeti lilidhihirisha viwango halisi (kwa msingi wa fomula ya moja kwa moja) vilivyopaswa kutumika kwenye vitu vya aina mbalimbali (vitabu, penseli, matengenezo, mitihani, n.k)

Kwa kweli, hii iliamua katika ngazi ya kati vipaumbele mahususi kwa ajili ya ngazi za wilaya na shule kuliko kuziwezesha shule zenyewe kuamua. Hili linaelekea kuwa kinyume na makusudi ya MMEM na kanuni za kukabidhi madaraka ya mpango wa ugatuzi.

Mwisho, ukweli kwamba fedha zilipelekwa na Wizara ya Elimu, na wala si TAMISEMI, unasisitiza uwezekano wa ukosefu wa uratibu miongoni mwa wizara mbalimbali zinazowajibika kwa kugharamia elimu.

**Nini Kifanyike?**

Kuzishughulikia changamoto hizi si kazi inayotisha kama inavyoonekana. Hayo mapendekezo manne hapa chini ni mikakati inayowezekana kwa kuhakikisha ulipaji kamili na unaobashirika wa fedha za ruzuku maalumu kwa kila mwanafunzi, ambao utasaidia kuongeza ubora wa elimu.

***1. Kiwango kamili cha ruzuku maalumu kwa kila mwanafunzi kinapaswa kupewa kipaumbele katika bajeti.***

Kiwango hiki cha malipo ya shs. 12,500 kwa mwanafunzi wa shule ya msingi – kinawezekana ndani ya viwango vya bajeti vilivyokadiriwa. Akiba inaweza kufanyika maeneo mengine yasiyo muhimu sana, kama vile masurufu, mikutano au magari. Data ya uandikishaji kuanzia 2007 itumike kwa kukokotoa kiwango cha kutumika kwa kila wilaya.

***2. Fedha zote zipelekwe kutoka kwenye wizara moja tu.***

Kwa jinsi hii, majukumu na uwajibikaji vitakuwa wazi. Kwa vile elimu ya msingi imekusudiwa kuwa wajibu wa serikali za mitaa chini ya ugawaji wa madaraka – kwa sera ya ugatuaji wa madaraka, ruzuku zote maalumu kwa kila mwanafunzi zitoke moja kwa moja kwa TAMISEMI.

***3. Kiwango cha kulipwa na utaratibu viwe wazi, vitangazwe na kufuatwa.***

Fedha zipelekwe mara mbili kwa mwaka – Shs. 6,250/= zipelekwe kwanza Septemba, na kiasi hichohicho kipelekwe tena Februari. Kupunguza malipo kuwa mara mbili

kwa mwaka kutaokoa kiasi kikubwa cha fedha katika gharama za uendeshaji. Kiasi hiki na utaratibu wa kuhamisha vitangazwe katika hotuba ya bajeti ya elimu Bungeni. Kwa jinsi hii, Wabunge, wazazi, walimu na raia wengine wanaohusika wanaweza kufahamu kuhusu haki zao na, hivyo, kufuatilia pale ambapo fedha hazipo.

***4. Mahitaji ya uwazi yawe bayana kwenye ngazi zote.***

Kuanzia hivi sasa, uhamishaji kutoka serikali kuu kwenda serikali za mitaa uchapishwe katika magazeti makuu na kwenye tovuti ya serikali.

Malipo kutoka wilayani kwenda mashirika pia yapatikane katika wilaya zote pamoja na tovuti ya TAMISEMI. Mwisho, kila shule itakiwe iweke kiasi kamili kilichopelekwa dhidi ya wanafunzi walioandikishwa au ahadi kwenye ubao wa matangazo wa umma au kwenye mlango wa ofisi ya walimu. Mwishoni mwa mwaka, ubao huohuo wa matangazo unapaswa uwe na taarifa kuhusu hali halisi ya matumizi ya fedha hizo. Kwenye ngazi zote, itolewe anwani moja ya mawasiliano kwa watu kufuatilia iwapo hawapati fedha.

---

[i] *Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi*

[ii] *Kila shule ya msingi ya Serikali inatakiwa iwe na akaunti mbili za benki – Akaunti ya Ruzuku Maalumu kwa kila Mwanafunzi na Akaunti ya Ruzuku ya Maendeleo (Study on Local Level Service Delivery, Decentralisation and Governance for JICA 2007, DEGE Consult)*

[iii] *Mfumo huu unapingana na sheria na taratibu zilizomo kwenye Mwongozo wa Fedha na Usimamizi wa Hesabu wa MMEM, ambao Kamati ya Maendeleo ya Elimu ya Msingi (BEDC) inapewa wajibu wa kukusanya rasilimali za Serikali na wafadhili, na Mhasibu Mkuu anatakiwa aiagize Benki ya Tanzania kuhamishia fedha shuleni na kwenye Halmashauri baada ya maombi toka kwa TAMISEMI.*

[iv] *Miongozo ya Bajeti ya Serikali za Mitaa, 2007/08*

SLP 79401 • Dar es Salaam • Tanzania
Simu (255 22) 2151852/3 • Faksi (255 22) 2152449
info@hakielimu.org • www.hakielimu.org

hakielimu